***Chagua majibu yaliyo sahihi kujaza mapengo 1 hadi 15.***

Uhai ni tunu ___1___ anayopewa mwanadamu na viumbe ___2___. Zawadi hii hutoka kwa Mungu pekee. Maisha ya binadamu huanza baada ya ___3___ za kiume kuungana na za kike na mtoto kuanza kukua katika tumbo la uzazi la mwanamke. ___4___ miezi tisa, mtoto ___5___ na mara moja anaanza kunyonyeshwa na ___6___. Haya ___7___ maziwa ya kwanza yenye uwezo wa kumkuza na ___8___ mwili wake uwezo wa kujikinga dhidi ya maradhi. Mtoto anastahili kunyonyeshwa kwa ___9___ kadhaa kabla ya ___10___ kupatiwa chakula cha aina nyingine yoyote.

Katika kukua kwa mtoto, anastahili ___11___ na kupewa haki zote za kimsingi. Ni vyema aonyeshwe ___12___ na alindwe kutokana na ___13___ zozote. Anapokua afundishwe kuwatii wengine na maadili ___14___ kwa jumla. Maadili hukuza mtoto akiwa mchanga kwani wahenga walinena ___15___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. adhimu | B. dhalimu | C. adimu | D. hadimu |
| 2. | A. zingine | B. nyingine | C. vingine | D. mwingine |
| 3. | A. jinsia | B. mbegu | C. nasaba | D. nyutu |
| 4. | A. Baada ya | B. Kabla ya | C. Badala ya | D. Fauka ya |
| 5. | A. huzaa | B. huzawa | C. huzalishwa | D. huzaliwa |
| 6. | A. mamawe | B. mamake | C. mamae | D. mamaye |
| 7. | A. ndio | B. ndiye | C. ndiyo | D. ndizo |
| 8. | A. kuupunguzia | B. kuundolea | C. kuupa | D. kuufanya |
| 9. | A. siku | B. miezi | C. majuma | D. miaka |
| 10. | A. kuanza | B. kutangulia | C. kuendelea | D. kukoma |
| 11. | A. kupuuzwa | B. kutelekezwa | C. kudunishwa | D. kutunzwa |
| 12. | A. mabezo | B. malezi | C. mavazi | D. mapenzi |
| 13. | A. dhuluma | B. maradhi | C. haki | D. tatizo |
| 14. | A. mbora | B. mabora | C. bora | D. ubora |

15. A. ukicha mwana kulia utalia wewe
    B. msafiri ni aliye bandarini
    C. udongo upatilize ungali maji
    D. asiyesikia la mkuu huvunjika guu

***Jibu maswali 16 hadi 30 kwa kufuata maagizo yaliyotolewa kwa kila swali.***

16. Tumia kiunganishi bora zaidi:-
Ningewasaidia sana maskini _____ ningekuwa tajiri.
A. lau
B. maadam
C. kwani
D. minghairi

17. Onyesha sentensi yenye ‘po’ ya masharti:
A. Ulipokalia painukie mara moja.
B. Watakuja kujuta wasipojihadhari.
C. Nilipofika alikuwa ameshaondoka.
D. Alipongezwa kwa kuupita mtihani.

18. Ni neno lipi linakamilisha sentensi kwa usanifu?
Babu yangu alikufa baada ya kuishi muda wa ______ saba.
A. Miaka
B. miongo
C. Karne
D. milenia

19. Jaza pengo kwa kivumishi mwafaka.
Alisafiri kwa kutumia baiskeli _______.
A. nzee
B. mzee
C. zee
D. lizee

20. Onyesha sentensi iliyo katika hali ya kutendesha:-
A. Aliozwa mke wiki iliyopita.
B. Mjakazi anaosha vyombo.
C. Dawa ilimlevya akawa hajijui.
D. Mama huuza bidhaa zake sokoni.

21. Onyesha kiwakilishi katika sentensi hii:
Nipe kiti hicho kilicho mbele yako, hiki kimevunjika.
A. hicho
B. mbele
C. yako
D. hiki


22. Mtu apitiaye makala yaliyoandikwa na kuyasahihisha huitwaje?
A. Mhariri
B. Mkalimani
C. Mhakiki
D. Mhasibu


23. Geuza sentensi hii iwe katika usemi halisi.
Alisema kuwa angesafiri keshoye ikiwezekana.
A. “Ningesafiri kesho ikiwezekana”, alisema. .
B. “Nitasafiri keshoye ikiwezekana,” alisema.
C. “Ningesafiri keshoye ikiwezekana,” alisema.
D. “Nitasafiri kesho ikiwezekana,” alisema.

24. Goti kwa mguu ni kama ______ kwa mkono.
A. bega
B. kiganja
C. kisugudi
D. kitengele


25. Onyesha sentensi yenye ‘ni’ ya kuelezea.
A. Tulipoitwa nilikimbia na kutoroka.
B. Ni nani asiyejua kusoma na kuandika?
C. Aliruka akajitumbukiza majini chumbwi!
D. Wanaomba sahani wapakuliwe chakula

26. Umbo lipi si mche?

A. 

B. 

C. 

D. 

27. Teua sentensi iliyo katika hali dunifu.
A. Chumba cha malazi ndicho kile.
B. Kiatu chake kimeng’arishwa.
C. Jambazi lile litatiwa nguvuni.
D. Watoto wadogo wasilewe pombe.

28. Pambo lipi huvaliwa nyweleni?
A. Ngeu
B. Kikuba
C. Kipuli
D. Kishaufu

29. Rehema ana mkono wa birika.
Maana yake ni nini?
A. Ni mwizi
B. Ni mchoyo
C. Ni mkarimu
D. Ni mtukutu

30. Onyesha sentensi yenye O-rejeshi ya awali.
A. Kalamu ambayo haiandiki haifai.
B. Shambani kulikolimwa kunapendeza.
C. Mwalimu asomeshaye ni stadi.
D. Kasisi aliwaombea waumini.

***Soma habari hii kisha ujibu maswali 31 hadi 40.***

Mwenyekiti wa Kamati Andalizi ya kongamano hili, mabibi na mabwana. Umaskini ndio tatizo kubwa zaidi barani Afrika. Je, maana yake halisi ni nini? Umaskini ni ile hali ya mtu kukosa chakula, makazi na uwezo wa kumiliki mali au kushiriki shughuli za kuzalisha mali. Nchini Kenya, mtu husemekana kuwa mkata iwapo pato lake ni chini ya shilingi 1239 kwa mwezi. Umaskini umetopea barani Afrika kiasi kwamba 60% ya wakazi wake wametota katika dimbwi la uchochole. Dhiki kubwa ya hali hii inapatikana majijini ambamo wengi wanaishi katika mitaa ya mabanda.

Kuna mambo mengi yanayochangia kuwepo umaskini. Moja ya mambo haya ni kuongezeka kwa idadi ya watu. Hivi sasa, kuna Waafrika milioni 800, wakiwemo Wakenya milioni 40. Jambo la pili, ni kuwa chumi zimeporomoka na mapato ya kitaifa ya nchi nyingi yamedidimia. Kwa hivyo, serikali zinashindwa kutoa huduma za kimsingi kama chakula, maji na afya kwa raia. Ili kujiokoa, nchi nyingi zinaamua kukopa kutoka nchi zilizoendelea. Baadaye, nchi za Kiafrika hulazimika kutumia fedha kidogo zinazopata kulipia riba huku wananchi wakiteseka. Hivi ninapozungumza, bara la Afrika lina deni la dola bilioni 300. Kati ya hizi, Kenya inadaiwa dola bilioni saba.

Bwana mwenyekiti, jambo la tatu lichangialo ufukara ni masharti yanayoambatana na mikopo. Nchi nyingi zimelazimishwa kuweka soko huru, kubinafsisha mashirika ya umma na kupunguza idadi za wafanyakazi. Matokeo ni kuwa bidhaa kutoka nje zinaangamiza viwanda. Tena nafasi za ajira sasa ni finyu hata vijana wenye shahada za vyuo vikuu leo wanasaga lami mitaani kutafuta kazi.

Umaskini Afrika pia unatokana na bei duni ya masoko ya nje. Bara la Afrika limekuwa likiuza rasilimali na mazao kwa nchi zilizoendelea kwa bei ya kijungu jiko. Hivyo, nchi za Afrika hazipati faida za kuweza kuimarisha hali ya maisha ya watu wake. Isisahaulike kuwa sisi wenyewe tunachangia umaskini. Hii ni kutokana na uongozi mbaya. Mipango ya maendeleo ya watawala wengi ni mibaya. Mfano wa hii ni ubadhirifu wa pesa kwa miradi ya fahari kama viwanda vya silaha ambavyo havina faida kwa raia.

Utawala mbaya husababisha masumbuko, chuki na uadui ambao huchochea migogoro na vita vya sisi kwa sisi. Jambo hili husababisha si tu uharibifu wa mali na mazingira, lakini vifo vya Waafrika wengi. Bila amani, shughuli za kuinua uchumi hukwama.

Sote twafahamu uovu wa rushwa. Lakini katika nchi nyingi za Kiafrika, ufisadi umejisimika vilivyo. Rasilimali ambazo zingewafaidi wote huporwa na kunufaisha vigogo wachache tu na vibaraka wao. Aidha majanga mengine husababisha umaskini. Baadhi ya haya ni matukio ya kimaumbile kama vile mafuriko, ukame na mitetemeko ya ardhi. Matukio haya huangamiza watu na kuharibu mali na miundo-msingi kama barabara. Hivi sasa, bara letu linakabiliwa na tisho kubwa; Ukimwi. Kila siku watu takriban 20000 wanapoteza maisha. Pesa nyingi zimetumiwa kugharamia matibabu, mazishi na kutunza mayatima.

31. Msemaji ametangulia mengine yote kwa kufanya nini?
A. Kuwatambua wasikilizaji
B. Kuwasabahi waliopo
C. Kuwaamkua na kuwazindua wahudhuriaji
D. Kuwakashifu walio mkutanoni

32. Kwa mujibu wa makala haya, umaskini si hali ya:-
A. mtu kukosa chakula
B. mtu kutokuwa na makazi
C. mtu kutoweza kumiliki mali
D. mtu kushiriki shughuli za kuzalisha mali.

33. Yote haya ni matokeo ya umaskini nchini Afrika isipokuwa:-
A. huduma za afya kukosekana
B. nchi zilizoendelea kutwaa mikopo
C. nchi za Afrika kujiingiza katika madeni
D. miradi ya maendeleo barani Afrika kuzorota

34. Masharti yanayoambatana na mikopo hudhamiria:-
A. kufanya mashirika ya kibinafsi yawe ya umma
B. kupigana vilivyo na umaskini
C. kupunguza idadi ya wafanyakazi wa kigeni
D. kuingiza bidhaa za kigeni katika nchi iliyokopa

35. Mwandishi angeweza kutumia msemo upi badala ya neno <u>'umetopea'</u> kwenye habari?
A. umekita mizizi
B. umepiga hatua
C. umepigwa vita
D. umetumbukia nyongo

36. Inamaanisha nini kusema <u>'nafasi za ajira sasa ni finyu'</u>?
A. zinapatikana kwa wingi
B. zimekosekana kabisakabisa
C. ni adimu mno
D. hazipendelewi tena na watu

37. Tatizo kuu linalokabili rasilimali za bara la Afrika ni lipi?
A. Masoko ya nje yawezayo kuuziwa hukosekana.
B. Hulazimika kuuzwa kwa bei duni sana.
C. Njia za kuzalisha rasilimali hizo hazipo kabisa.
D. Uagizwaji wa rasilimali za nchi za nje.

38. Lipi kati ya mambo yafuatayo si sera ya utawala mbaya?
A. Uwepo wa viwanda vya kifahari
B. Masumbuko, chuki na uadui
C. Shughuli za kuinua uchumi kukwama
D. Viongozi kujinufaisha kwa mali ya umma

39. Kulingana na habari, ipi si sababu inayochangia umaskini barani Afrika?
A. Mizozo na vita vya wenyewe kwa wenyewe
B. Majanga ya kiasili
C. Upungufu wa mikopo inayotoka nje
D. Uongozi usio na uwazi na uwajibikaji

40. Mzungumzaji wa makala haya ameangazia umaskini barani Afrika kwa njia ya:-
A. malumbano
B. utenzi
C. mhadhara
D. mjadala

**<u>Soma habari hii kisha jibu maswali 41 hadi 50.</u>**

Siku moja Juma aliporudi kutoka shuleni, aliwakuta watu wengi wenye nyuso zilizokunjana wamesimama karibu na lango la babu yake. Nyumba ya babu yake ilikuwa imeungua moto. Juma aliweza kuona makaa na jivu tu.

Hapo alishtuka sana kwa maana alijua bayana kuwa si jengo tu lililoungua, bali hata vitu vyote vilivyokuwemo ndani. Machozi yalimtiririka michirizi michirizi alipowaza na kuwazua jinsi angepata chakula na mahali pa kulala. Akamwuliza babu yake kwa jitimai "babu , kuna vitu vilivyosalia?"

Mzee Kazamwendo alimtazama kwa huzuni kisha akamjibu, "mjukuu wangu, Juma, ni vitu vichache tu tulivyofaulu kuvitoa nje lakini vingine vyote vimeteketea kabisa." Kisha aliyaelekeza macho mahali palipokuwa na vigae vya chungu ambacho kiliteketea katika moto ule. Akachukua vile vigae kisha akasema, "Juma, waona vigae hivi vya chungu?" Juma akajibu, "naam, babu."

Kazamwendo akaendelea, "kilikuwa chungu ambamo nilitia fedha za sarafu na noti ambazo nilizidunduliza kila wiki. Nilikuwa nikizipata kwa kuuza pamba. Ingawa pengine nilipata fedha kichele tu, sikufuja mali ila nilijinyima mengi na kuziweka ili zinifae wakati wa dhiki. Nilikuwa nikikumbuka methali isemayo, "akiba haiozi." Chungu hicho nilikificha darini ili kisifikiwe na mtu yeyote. Sasa nimekuwa fukara fakiri.

Juma alipotaka kujua ni pesa ngapi babu yake alikuwa akiziweka kila juma na kwa muda gani, alimjibu kuwa alikuwa akiweka shilingi elfu tano kila wiki kwa muda wa miaka minne. Juma akasema, "babu, uliamua vyema kujiwekea fedha ila hukujua mahali salama pa kuziweka fedha hizo."

Kusikia haya, Mzee Kazamwendo <u>akashika tama</u> na akaketi chini ya kivuli huku amekunja uso ambao ulikuwa na makunyunyu kama ngozi ya kifaru. Kisha akamwelekea Juma akamwuliza, "umesema sikujua mahali salama pa kuweka fedha hizo? Ningeziweka wapi? Tangu zama za baba na babu zetu walioanza kutumia pesa hakuna aliyeziweka kwa namna nyingine ila kuziweka katika chungu au kuzichimbia chini ardhini. Pukachaka! Sasa wataka kuniambia nini mtoto wa jana?" Mzee alikuwa amepandwa na mori kweli.

Juma akainamisha kichwa chini kama mtu anayefikiria kujibu, bila kukawia akasema, "babu, kunradhi! Sikuwa na maana ya kukudharau, hata! Ila siku hizi kuna njia bora zaidi za kujiwekea akiba." Juma akapata wakati mwafaka wa kumwelimisha babu. Akamwambia kuwa njia mojawapo ni kuziweka benkini kwa sababu hazitaibwa na utakuwa ukipata riba baada ya kila mwaka.

Mzee Kazamwendo akamshukuru mjukuu wake kwa kumwelimisha. Juma akamtuliza babu yake akasema, " ingawa majuto ni mjukuu, hakuna marefu yasiyo na ncha. Iwapo tutaziweka fedha zetu benkini, jasho letu halitazidi kupotea."

Mwaka uliofuata baada ya kupitia kipindi kigumu cha kukirimiwa na wahisani akaenda kuziweka fedha katika benki. Tangu wakati huo hakuwa na kiherehere kwani fedha zake zilikuwa salama u salimini.

41. Watu walikuwa na nyuso zilizokunjana kwa sababu:-
A. walikutwa na Juma alipotoka shuleni
B. walikuwa karibu na lango la babu
C. nyumba ya babu ilikuwa imeungua moto
D. Juma aliweza kuona makaa na jivu tu.

42. Kwa nini machozi yalimtiririka Juma michirizi michirizi?
A. Alililia fedha nyingi alizopoteza babu.
B. Alihofia dhiki ambayo alifahamu angeipitia.
C. Alihurumishwa na wazo la babu angekula nini na kulala wapi.
D. Alijiunga na babu na wengine kulilia janga lililozuka.

43. Iwapo mwaka mmoja una wiki hamsini na mbili, basi ni pesa ngapi alizokuwa amehifadhi babu kwenye chungu kabla ya mkasa wa moto?
A. Shilingi milioni moja na laki nne.
B. Shilingi mia moja na nne elfu.
C. Shilingi milioni moja na elfu arubaini.
D. Shilingi elfu mia mbili na sitini.

44. Ni hakika kwamba babu alipoweka fedha kwenye chungu na kukificha darini:-
A. alipuuza uhifadhi wa pesa kwenye benki
B. hakuamini haba na haba hujaza kibaba
C. alimfahamisha mjukuu wake ni kiasi gani
D. hakuhofia kupoteza akiba yake.

45. Mwandishi ametumia msemo <u>'akashika tama'</u> kumaanisha:-
A. akashangaa
B. akakasirika
C. akanyamaza
D. akahuzunika.

46. Kwa nini babu alipandwa na mori?
A. Alihisi mjukuu wake alimdharau na kumdunisha.
B. Alikumbuka kiasi kikubwa cha pesa alichopoteza.
C. Alijuta kwa nini hakuzifadhi pesa zake vyema zaidi.
D. Aliwalaumu babu zake waliomfunza njia mbovu ya kuhifadhi pesa.

47. <u>'Pukachaka!'</u> Hicho ni kihisishi kinachodhihirisha:-
A. dharau
B. hasira
C. kuchoka
D. kushangaa

48. Maneno ya Juma hayathibitishi kwamba alikuwa mwenye:-
A. heshima na adabu
B. akili tambuzi na ujuzi
C. utovu wa staha na nidhamu
D. moyo safi wenye huruma

49. Moto uliozuka ulisababisha hasara lakini ukaacha funzo. Hilo linamaanisha japo mambo mabaya yana madhara wakati mwingine huwa na faida fulani kwa yule aliyepatana nayo. Ni methali ipi inayotoa funzo hili?
A. Hakuna msiba usio na mwenziwe.
B. Uzuri wa kuyu ndani mabuu.
C. Baniani mbaya kiatu chake dawa.
D. Hakuna zuri lisilokuwa na doa.

50. Kiini kikuu cha habari hii ni kutuzindua tufahamu:-
A. jinsi ya kuhifadhi pesa zetu
B. kuwa baadhi ya tamaduni zimepitwa na wakati
C. kwamba tunapaswa kuwaelimisha wazee wetu
D. teknolojia ya kisasa ina faida na madhara pia.